*Kioo cha Lugha, Juz. 19(1), 2021, 161-179*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Usawiri Kijinsia wa Dhamira katika Misemo ya kwenye Vyombo vya Usafiri nchini Tanzania na Dhima zake kwa Jamii

*Shani Omari Mchepange*[1]

## Ikisiri

Usawiri kijinsia ni mojawapo ya mada maarufu katika kazi za fasihi andishi na fasihi simulizi. Makala hii hailengi kuchunguza suala hili katika matini za kifasihi zilizozoeleka kuchunguzwa na watafiti mbalimbali kama vile riwaya, tamthilia, ushairi, hadithi na kadhalika. Lengo la makala hii ni kuchunguza usawiri wa kijinsia kupitia dhamira zinazopatikana katika misemo inayoandikwa katika vyombo vya usafiri nchini Tanzania. Eneo hili halijapewa aula miongoni mwa wahakiki wa fasihi ya Kiswahili wa masuala ya kijinsia. Data za makala hii zimekusanywa uwandani katika sehemu mbalimbali za jiji la Dar es Salaam kwa njia ya ushuhudiaji wa misemo iliyoandikwa katika vyombo hivi kama vile daladala, malori, bajaji, bodaboda na baiskeli. Aidha, data zilikusanywa kutoka katika matini andishi, tovuti, makundi ya kijamii kama vile *WhatsApp* na *Facebook* na usaili kwa baadhi ya madereva, makondakta na watumiaji wa vyombo hivi. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Kilongo Tunduizi wa Kifeministi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba misemo hii inasawiri masuala ya kijinsia kupitia dhamira mbalimbali kama vile mapenzi na ndoa, tabia na wajihi, uchumi na elimu. Usawiri huu kwa kiasi kikubwa unatweza jinsia moja na kukweza jinsia nyingine. Kutokana usawiri huo, mtazamo (wa jamii) kuhusu wanawake unapaswa kubadilika ili kuleta usawa wa kijinsia. Aidha, usawiri huu una dhima mbalimbali ikiwamo kuendeleza utamaduni wa jamii na kusawiri ukweli fulani wa maisha.

## 1.0 Utangulizi

Kushamiri kwa tafiti kuhusu masuala ya kijinsia katika nyanja mbalimbali katika karne ya 21 ni matokeo ya mikutano kadhaa ya kimataifa ya wanawake duniani. Mikutano hiyo ni pamoja na ule wa Mexico wa mwaka 1975, Copenhagen mwaka 1980, Nairobi mwaka 1985, na Beijing mwaka 1995. Mathalani, mkutano wa

[1] Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: shaniom@yahoo.co.uk

wanawake uliofanyika Beijing ulisisitiza zaidi usawa wa kijinsia kuanzia ngazi za chini hadi za kimataifa (Erlurk, 2004). Makala hii ni mwendelezo wa makala nyingine kadhaa kuhusiana na usawiri kijinsia wa masuala mbalimbali katika kazi za fasihi na sanaa. Kwa umahususi, lengo la makala hii ni kuchunguza namna dhamira zinazozungumziwa kwenye misemo inayoandikwa katika vyombo vya usafiri nchini Tanzania inavyosawiriwa kijinsia.

Usawiri au uwakilishi kijinsia umetafitiwa katika nyuga mbalimbali, kama vile elimu, ajira, malezi, afya, siasa, utamaduni, uchumi, fasihi na mitandao ya kijamii (taz. Meena, 1996; Mbilinyi, 2000; Howard na Rackin, 2002; Sen, 2002; Waylen, 2007; Mosha, 2013; Lyimo, 2014; Mosha, 2019; Ligaga, 2020). Kwa kiasi kikubwa, tafiti hizi mbali na kuonesha changamoto katika masuala ya kijinsia katika nyanja mbalimbali, zinasisitiza haja ya kuwapo kwa usawa wa kijinsia. Nchini Tanzania, tafiti za kifasihi kuhusu masuala ya kijinsia zimezoeleka kufanyika kupitia tanzu zake kama vile riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Hata hivyo, lengo la makala hii ni kuchunguza usawiri wa kijinsia kupitia dhamira zinazopatikana katika misemo inayoandikwa katika vyombo vya usafiri. Tafiti katika vyombo vya usafiri zimebaini kwamba vyombo hivi vina dhima kubwa si tu katika kusafirisha watu na bidhaa zao, bali pia kusambaza maarifa kuhusu masuala mbalimbali katika jamii kupitia misemo yake (taz. Lawuyi, 1997; Wa-Mungai, 2003; Rassmann, 2004; Mahenge, 2009; Mturo, 2011; Omari, 2011). Mathalani, Wa-Mungai katika utafiti wake nchini Kenya, amebaini pamoja na mambo mengine kwamba, kupitia stika, muziki unaopigwa, lugha ya makondakta na semi zinazoandikwa, matatu (daladala) ni kipengele muhimu cha utamaduni miongoni mwa watumiaji wake. Nao Mahenge na Mturo wakichunguza fani na maudhui katika semi za kwenye daladala nchini Tanzania, wanabaini kwamba zinatumia mbinu mbalimbali za kifani kama vile lugha ya kitamathali na wahusika katika kuibua dhamira kama vile imani kwa Mungu, elimu, mapenzi, maradhi ya UKIMWI, maadili, umuhimu wa kufanya kazi, umaskini na umoja na mshikamano. Nchini Tanzania vyombo hivi vya usafiri, kwa kiasi kikubwa,vinaendeshwa na wanaume (madereva, makondakta, wapiga debe na wamiliki), hali hii inatupa hamasa ya kutafiti dhamira za misemo inayoandikwa katika vyombo hivyo kwa mrengo wa kijinsia.

Jinsia kwa mujibu wa UNESCO (2003) inahusu wajibu na majukumu ya wanaume na wanawake ambayo yanaundwa katika familia, jamii na utamaduni wa jamii husika. Dhana hii ya jinsia pia inahusu matarajio kuhusiana na sifa, uwezo na tabia ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Nao World Bank (2012) wanafasili kwamba jinsia ni kaida na itikadi zinazoundwa na jamii ambazo zinaukilia matendo na mwenendo wa wanaume na wanawake. Nayo misemo ni tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali kuelezea kitu au wazo kwa ufupi (Mturo, 2011). Misemo ni semi zinazoibuka kwa muda fulani kwa madhumuni maalumu na kuenea katika jamii na kisha kutoweka au kubadilika au kubakia katika kumbukumbu za watu kwa muda mrefu (Mulokozi, 2017). Hivyo, katika makala hii misemo inayochunguzwa ni zile

matini au tungo fupifupi ambazo zimeandikwa katika vyombo vya usafiri. Dhamira ni wazo kuu ambalo linazungumziwa katika kazi ya fasihi. Maswali yanayojibiwa katika makala hii ni mawili: Dhamira zinazowasilishwa katika misemo hiyo zinasawiriwaje kijinsia? Misemo hiyo ina dhima gani kwa jamii?

Data za uwandani za makala hii zimekusanywa kati ya mwaka 2018 na 2020 kwa njia ya ushuhudiaji wa misemo iliyoandikwa kwenye vyombo vya usafiri katika sehemu mbalimbali za jiji la Dar es Salaam. Maeneo hayo ni kama vile Ubungo, Mbezi, Buguruni, Kariakoo, Temeke, Mbagala, na Mwenge. Vyombo vya usafiri vilivyolengwa ni daladala, malori, bajaji, bodaboda na baiskeli. Kwa kutumia usampulishaji fursa, mtafiti alishuhudia misemo katika vyombo hivyo kwa kadiri alivyokutana navyo na kisha kunukuu baadhi ya misemo iliyoandikwa humo inayoendana na mada ya utafiti wake. Misemo mingine ilikusanywa kutoka katika matini andishi tangulizi[2], tovuti[3] na mitandao ya kijamii kama vile *WhatsApp* na *Facebook*. Mtafiti pia alifanya usaili na madereva, makondakta na abiria wa vyombo hivyo.

Makala hii imegawanyika katika sehemu nne: Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambayo inaeleza madhumuni ya makala, inatoa fasili za msingi za dhana ambazo zimejadiliwa katika makala hii na kueleza mbinu za utafiti. Sehemu ya pili inafafanua nadharia ambayo imeongoza uchambuzi wa data za makala hii. Sehemu ya tatu ni uchambuzi wa data kuhusu usawiri kijinsia wa dhamira zinazojitokeza katika misemo inayopatikana katika vyombo vya usafiri pamoja na dhima ya misemo na usawiri huo kwa jamii. Sehemu ya nne ni hitimisho la makala.

## 2.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Kilongo Tunduizi wa Kifeministi[4] (kuanzia sasa UKTF) (Lazar, 2007). Kwa mujibu wa Lazar, ambaye ni mwasisi wa nadharia hii, UKTF unahusu uchambuzi wa lugha na kilongo kwa kufuata taaluma ya ufeministi, jinsia na wanawake; yaani inatambua umuhimu wa lugha na taaluma ya kilongo katika uchunguzi wa masuala ya kifeministi katika jinsia na taaluma ya wanawake. Aidha, UKTF unaonesha mahusiano baina ya jinsia, mamlaka na itikadi katika matini andishi au simulizi katika jamii husika. UKTF unapinga vilongo ambavyo vinatetea mfumodume (mfumo unaompendelea mwanaume na kumtenga au kumdunisha mwanamke) na unataka mabadiliko (Lazar, 2005 katika Lazar 2007). Kilongo ni namna watu wanavyotumia lugha katika matini na miktadha mbalimbali. Kupitia kilongo, watu wanawasilisha dunia yao, hoja zao, matendo yao, utambulisho na mahusiano yao kwa wengine, na wanashiriki katika vitendo na mtagusano na wengine (Schiffrin, 2006). Nadharia hii imetusaidia kuchambua usawiri kijinsia wa dhamira zinazopatikana katika misemo ya kwenye vyombo vya usafiri,

[2] Taz. Ponera na Kikula (2017).
[3] Taz. Kaijage (2016).
[4] Feminist Critical Discourse Analysis (Feminist CDA).

mahusiano ya kijinsia, nafasi yake katika kuendeleza au kupinga mamlaka, itikadi na mitazamo ya wanajamii. Katika makala hii tunajenga hoja kwamba misemo iliyoandikwa kwenye vyombo vya usafiri ni elementi muhimu katika mjadala kuhusu masuala ya kijinsia na inachangia sana katika kusawiri utambulisho wa kijinsia.

## 3.0 Uchambuzi wa Data

Katika utafiti huu jumla ya misemo thelathini na sita (36) ilikusanywa kutoka uwandani, tafiti tangulizi na mitandaoni. Misemo hiyo imeandikwa kwa Kiswahili na ni ile inayodokeza au kutaja jinsia ya kike na/au ya kiume na/au sifa ambazo zinaambatana nazo.

### 3.1 Dhamira Zinazozungumziwa na Usawiri wake Kijinsia

Dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Pia, ni suala linalokuzwa na kuendelezwa na msuko pamoja na mahusiano na wahusika katika kazi ya fasihi (Wamitila, 2003). Dhamira zinazozungumziwa katika misemo hiyo na namna zinavyosawiriwa kijinsia tunaweza kuzigawa katika makundi makuu mawili: mapenzi na ndoa, na mapenzi na elimu kwa mtoto wa kike. Dhamira ya mapenzi na ndoa tumeigawa[5] katika dhamira ndogondogo ambazo ni kuchagua mwenzi wa kuoa, kuachwa na kufa, tabia na wajihi, nafasi ya wapenzi wengi, na uwezo wa kiuchumi na kumiliki mali. Kimsingi, kama wasemavyo Howard na Rackin (2002:39) ni ‘vigumu kuzungumzia jinsia bila ya kugusia nyanja nyingine za kijamii, kwani jinsia ni kigeu kinachojenga historia na kinatambua mahusiano yake na nyanja nyingine za maisha kama vile uchumi, siasa na utamaduni.’ Hivyo, uchambuzi wa swali la kwanza umelenga kubainisha dhamira hizo na usawiri wake kijinsia, yaani namna zinavyomchora mwanamke na mwanaume.

#### 3.1.1 Mapenzi na Ndoa

Misemo mingi katika data zilizokusanywa inazungumzia masuala ya mapenzi na ndoa. Kusisitizwa kwa suala la ndoa katika misemo hii kunaonesha umuhimu wa ndoa katika jamii za Kiafrika (taz. Mbiti, 1995), ikiwamo Tanzania. Misemo hii inaonesha majukumu, wajibu, sifa na tabia ya mwanamke na mwanaume katika masuala ya mapenzi na ndoa, kama ifuatavyo:

##### 3.1.1.1 Kuchagua Mwenzi

Misemo kadhaa inayopatikana katika vyombo vya usafiri inayohusu mapenzi na ndoa inagusia suala la uchaguzi wa mwenzi. Mathalani, msemo ‘Mapenzi bila uongo humpati mtu’ ingawa haubainishi wazi jinsia inayolengwa, unaonesha kwamba jinsia zote mbili hutumia uongo ili kumpata mpenzi. Mmojawapo wa watoataarifa anaeleza kwamba kama ukweli ungekuwa unatumika wakati wote katika kutongoza mwenzi au mahusiano ya kimapenzi, basi watu wengi wasingekuwa na wenzi walionao sasa.

[5] Mgawanyo huu tumeufanya ili kurahisisha uchambuzi wetu wa data, kwani data zake zinaingiliana kwa kiasi kikubwa.

Hivyo, kwenye mapenzi kuna uongo ndani yake. Mbali na msemo huu, misemo mingine inasisitiza kuwa na umakini katika uchaguzi wa mwenzi wa kuoa au kuolewa naye. Kwa mfano, msemo ‘Ajali si kugongwa na gari tu hata ukikosea kuoa/kuolewa, nayo ni ajali’. Ndoa nyingi huvunjika kutokana na wanandoa kutofahamiana vizuri kabla ya kuoana. Huu ni msemo wa kiushauri kwa watu wa jinsia zote ambao wanataka kuoa au kuolewa. Mbali na msemo huu ambao unalenga jinsia zote, mifano zaidi imebainika kumlenga mwanaume kuwa makini zaidi katika uteuzi wa mwenzi. Misemo hiyo ni ‘Heri kukosea kujenga nyumba kuliko kukosea kuoa’ na ‘Usichague mke kwenye sherehe’. Ikizingatiwa kwamba mwanaume ndiye anayeposa na kutoa mahari; msisitizo unatolewa kuhusu kuchagua mke. Aidha, misemo hii inaonesha umuhimu wa ndoa katika jamii. Msemo kuhusu sherehe unadokeza utamaduni wa mwanamke kujipamba katika sherehe kiasi cha kuonekana mzuri wa sura kumbe sivyo alivyo. Kwa ujumla, misemo hii kama anavyoeleza Lazar (2005) ni vilongo vinavyoakisi mahusiano na maadili ya kijamii. Hivyo, kupitia misemo hii, ushauri unatolewa kwa mwanamke na mwanaume kuwa makini katika uchaguzi wa mwenzi ili kupata mke au mume faafu.

### 3.1.1.2 Kuachwa na Kufa

Usawiri kijinsia katika mapenzi na ndoa kwenye misemo ya vyombo vya usafiri unazungumzia pia suala la kuachwa na kifo. Mfano wa misemo hiyo ni ‘Mtalaka wa huku ndo mke mpya wa kule’ na ‘Kuachwa na mwanamke anayependa hela ni sawa na kumaliza mkopo benki.’ Misemo hii inaonesha tabia ya kuachana katika mahusiano ya kimapenzi; wote, mwanaume na mwanamke, wamepewa uwezo wa kutaliki mwenzi. Katika msemo wa kwanza mwanaume ndiye anayeacha (kutoa talaka) na kisha kumpa fursa mwanamke aliyeachwa kuolewa na mume mwingine. Msemo huu unafanana na msemo maarufu wa Kiswahili usemao ‘Wewe ukisema cha nini wenzio wanasema nitakipata lini’. Katika msemo wa pili mwanamke mpenda pesa anapewa uwezo wa kuacha mume au bwana na hata kutafuta bwana mwingine. Misemo hii kwa kiasi fulani inamsawiri mwanamke kuwa ni mwenye thamani ya kuweza kuolewa tena baada ya kuachwa na ana uwezo wa kuipata na kuitumia pesa kutoka kwa mwenzi wake wa kiume kiasi cha mwanaume huyo kufurahi kuachwa na mwanamke huyo. Hata hivyo, hadi mwanamke huyo kuachwa inaonesha kwamba alikuwa na kasoro fulani pia anakera kwani anapenda sana pesa.

‘Nikifa mke wangu asiolewe: usia uheshimiwe’ ni msemo mwingine. Msemo huu kwa upande mmoja unaonesha mapenzi ya mume kwa mke wake kiasi cha kutaka mke huyo asiolewe na mtu mwingine pindi akifa. Vilevile, msemo huu unaonesha tabia njema ya mke wake kiasi kwamba anaona wivu akiishi na mume mwingine baada ya kifo chake. Msemo huu pia, kwa kurejelea Lazar (2007:148), unaonesha ‘mahusiano ya kimamlaka na utawala’ ambapo mwanaume anaonekana ana mamlaka makubwa kwa mkewe kiasi cha kuonesha raghba ya kuendelea kummiliki mke huyo hata kama akifa. Mume huyo, labda kutokana na kumlipia mahari mke huyo, anaona kuwa ni mali yake hivyo anausia asiolewe tena. Anataka wosia huo uheshimiwe na mke na familia husika. ‘Wosia ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake kuonesha nia

yake jinsi gani angependa mali yake igawanywe baada ya kufa kwake' (TLS, 2015:12). Ujumbe uliopo kwenye msemo huu mbali na kuonesha mapenzi aliyonayo mume kwa mkewe, pia unaendeleza mfumodume kwani mwanaume anaonekana ni mwenye mamlaka kimaamuzi na mmiliki mali, ikiwamo mke. Kwa mujibu wa Ackermann (1991 katika Katambi, 2021) mfumodume ni utawala wa baba. Mwanaume ambaye ndiye mkuu wa familia huwa na mamlaka ya juu kisheria, kiuchumi na kijamii kuliko mwanamke.

Suala la kifo pia limezungumziwa kupitia kutoa mimba kunakofanywa na baadhi ya wanawake katika msemo 'Kutoa mimba haikufanyi kuwa msichana bali utabaki kuwa mama wa marehemu'. Utoaji mimba huchochewa na sababu mbalimbali ikiwamo kukimbiwa na mwenzi, kupata mimba bila ya kutarajia, na maradhi. Sababu nyingine kwa mujibu wa baadhi ya makondakta na madereva ni kwamba wasichana wengi hawataki kupoteza usichana wao kwani wanaona kwamba kubeba mimba ni kuelekea uzeeni. Msemo huu unatoa tahadhari kwa wasichana watoao mimba kwani kufanya hivyo hakuwarudishii usichana wao bali huwageuza kuwa mama wa marehemu. Kimsingi msemo huu unapinga suala hili la utoaji wa mimba kwani kidini kutoa mimba ni dhambi na ni ukatili wa kibinadamu.

### 3.1.1.3 Tabia na Wajihi

Suala la mapenzi na ndoa limezungumziwa pia kupitia tabia na wajihi (mwonekano) wa mwanamke na mwanaume. Mathalani, msemo 'Kuoa mke mweupe ni kama kupanda miwa eneo la shule' na 'Kuoa mke mzuri ni sawa na kulima miwa eneo la shule' inaonesha kwamba weupe na uzuri ni mambo yanayowavutia baadhi ya wanaume. Mathalani, ni jambo la kawaida kukuta baadhi ya wanawake wakiutafuta weupe kwa kunywa vidonge au kujichubua sura au mwili kwa dawa bila ya kujali madhara wanayoweza kuyapata (taz. Omari na Senkoro, 2018). Kumlinganisha mwanamke mweupe au mzuri na miwa iliyopandwa eneo la shule kunaonesha mwanamke huyo hutongozwa na wanaume wengi, hatimaye hushawishika kimapenzi na 'huliwa' na wanaume hao kama miwa ambayo imepandwa katika eneo la shule inavyoliwa na wanafunzi. Kwa upande mmoja, mwanamke mweupe na mzuri anasawiriwa kama ni rahisi kutongozeka kimapenzi na kwa upande mwingine, misemo hii inaonesha usumbufu wa wanaume kimapenzi kwa wanawake wazuri na weupe.

Msemo mwingine ni 'Mwanamke sura, tabia nitamnyoosha.' Msemo huu, kama ilivyo misemo iliyotangulia, unaonesha baadhi ya wanaume kupenda wanawake wenye sura nzuri. Mwanaume huyo yuko tayari kurekebisha tabia mbaya ya mwanamke huyo ili mradi tu ana sura nzuri. Kurekebishwa huko kunaweza kuwa kwa kumwelekeza, kumpiga na kadhalika. Msemo mwingine kuhusu uzuri wa mwanamke ni 'Uzuri wa mwanamke tabia, sura hata mbuzi anayo'. Msemo huu wenye lugha ya ucheshi unaonesha umuhimu wa tabia kwa mwanamke, kwani sura si jambo la msingi hata mbuzi anayo. Msemo huu unasisitiza msemo wa Kiswahili usemao 'Uzuri wa mwanamke si sura ni tabia.' Suala la mwanamke mzuri ni yupi katika misemo hii

linaonesha utambuzi na mitazamo tofauti ya wanaume kuhusu wanawake wawapendao; kuna wale wanaopenda sura na wale wanaopenda tabia.

‘Kahaba hana mahaba’ na ‘Kama mzuri olewa’ ni misemo mingine inayosawiriwa kijinsia katika mapenzi na ndoa kwa upande wa tabia na wajihi. Kahaba huchukuliwa na wengi kuwa ni mwanamke anayefanya ngono kwa ajili ya kujipatia kipato. Msemo wa kwanza ingawa unaonesha kwamba mwanamke anajitafutia kipato chake ili kujikimu kimaisha, kipato hicho hata hivyo kinatokana na kazi isiyo halali, ukahaba. Nchini Tanzania ukahaba si kazi halali. Msemo wa pili unasisitiza umuhimu wa kuolewa kwa mwanamke kwa hiyo unamkebehi mwanamke ambaye amechelewa kuolewa kutokana na sababu mbalimbali. Katika jamii, ingawa wote mwanamke na mwanaume wanapaswa kuoa au kuolewa, lakini mwanamke akichelewa kuolewa huonekana kama ana kasoro fulani na hata kukebehiwa na baadhi ya watu. Kuolewa ni heshima kwa mwanamke. Mshangao kwa msichana mzuri kutoolewa unaelezwa pia na wimbo wa Daudi Kabaka uitwao ‘Msichana wa Elimu’. Mstari mmojawapo katika wimbo huo unasema, ‘Msichana wa sura nzuri, kitu gani kinakufanya usiolewe’ (Kabaka, h.t).

Misemo mingine inamuonesha mwanamke kuwa mwenye tabia ya kupenda pesa na mali. Suala hili linapatikana katika msemo ‘Filisika ujue tabia ya mkeo’. Msemo huu haueleza wazi kinachotokea baada ya mume kufilisika lakini baadhi ya watoataarifa wetu wanaeleza kuwa mwanamke huyu anaweza kudai talaka au kutengana na mumewe, kuwa na wapenzi wengine na hata kumdharau mumewe. Tabia ya mwanamke inadokezwa pia kupitia msemo ‘Mkanye mkeo gari sio langu’. Msemo huu unaonesha kwamba mwanamke huyu mume wake hana gari hivyo ametokea kumpenda mwanaume mwenye gari, hata hivyo, mwanaume huyo gari hilo si lake bali yeye ni dereva tu. Hivyo, bwana huyo dereva anamweleza mume wa mke huyo kwamba amkanye mke wake maana yeye gari si lake. Misemo hii si tu inaonesha mwanamke anapenda wanaume wenye pesa na mali, bali pia inadokeza kuwa ana tamaa, anapenda anasa, malaya (taz. pia Mbughuni, 1982; Ngongolo, 2015) na si mvumilivu pindi mume wake anapoyumba kiuchumi. Kwa ujumla, misemo hii inaonesha ‘mitazamo ya mtu binafsi au tabia za watu’ katika jamii (Lazar, 2007).

Aidha, misemo ‘Kama mapenzi ni pesa kaolewe na benki’ na ‘Usinichune sana nina watoto’ inazidi kuonesha kuwa mwanamke ana tabia ya kupenda pesa na/au hana mapenzi ya dhati. Msemo wa kwanza unaonesha hasira ya mwanaume kwa mwanamke aliyempenda lakini mwanamke huyo anaweka pesa mbele, hivyo, anaona ni vema akaolewe na benki kwani ndiyo sehemu inayotunza fedha; kwa hiyo, atapata kiasi chochote akitakacho. Katika msemo wa pili, mwanaume si tu anajua kwamba analiwa pesa zake na mwanamke wake, bali pia anaonesha tabia ya wanawake kupenda pesa na mali. Wakati huohuo mwanaume huyo anatambua nafasi yake kwa malezi ya watoto wake. Hivyo, anamsihi mwanamke huyo amchune kwa kiasi.

Tabia nyingine kuhusiana na mwanamke kupenda pesa inapatikana katika msemo ‘Kuachwa na mwanamke anayependa hela ni sawa na kumaliza mkopo benki’. Mwanamke mpenda pesa ni mzigo kwa mwanaume, ni sawa na kuwa na mkopo benki

ambao unapaswa kulipwa kila mwezi. Mwanaume anaonesha furaha yake akiachwa na mwanamke huyo kama anavyofurahi amalizapo mkopo wa benki. Kwa upande mwingine msemo huu unamsawiri mwanamke kuwa ni mnyonyi wa mali za mwanaume. Aidha, inaonekana kuwa wanaume wa leo hawapendi wanawake wa aina hii; wanapenda wanawake wanaojituma na kusaidiana nao katika kutafuta pesa. Aidha, misemo hii haioneshi tu tabia ya mwanamke ya kupenda wanaume wenye mali na pesa, bali pia inaonesha kwamba wamiliki mali na wenye uwezo wa kiuchumi ni wanaume. Kwa kiasi kikubwa misemo hii inaonesha upande hasi wa jinsia ya kike kwamba mwanamke: anapenda ngono, ana tabia mbaya, anapenda pesa na kadhalika, jambo ambalo nadharia ya UKTF inataka mabadiliko katika usawiri huu wa kijinsia (Lazar, 2007). Tazama vielelezo vifuatavyo kwa baadhi ya misemo[6] hiyo.

<table>
<tr><td>
</td><td>
</td></tr>
<tr><td>a. Kuachwa na mwanamke anayependa hela ni sawa na kumaliza mkopo benki</td><td>c. Kutoa mimba haikufanyi kuwa msichana bali utabaki kuwa mama wa marehemu</td></tr>
<tr><td>
</td><td>
</td></tr>
<tr><td>b. Usinichune sana nina watoto</td><td>d. Filisika ujue tabia ya mkeo</td></tr>
</table>

***Kielelezo Na. 1: Misemo kwenye malori (a, b, c) na daladala (d)***

Tabia nyingine kuhusu mwanamke inajitokeza kupitia msemo ‘Nyumba ndogo haili matembele’. Matembele ni aina ya mboga ya majani ambayo kwa kawaida si ghali. Msemo huu unaonesha tabia ya wanawake vimada (nyumba ndogo) kwamba wanapenda maisha ghali. Msemo unawaasa wanaume kwamba ‘nyumba ndogo’ wana gharama kubwa ya kuwahudumia si sawa na mke ambaye anaweza kuvumilia hali ngumu katika maisha ya ndoa. Nyumba ndogo wengi hupenda vyakula, mavazi, nyumba, starehe, na vitu mbalimbali vya gharama kubwa.

Aidha, zipo tabia kadhaa kuhusu wanaume ambazo zinazungumziwa katika misemo hii. Mathalani, msemo ‘Ukitaka kumjua mume mwenzio, muachie mkeo’ unadokeza tabia ya baadhi ya wanaume kupenda wake wa wanaume wenzao. Msemo

[6] Picha zote zimepatikana kutoka makundi mbalimbali ya *WhatsApp*.

unalenga kumpima mwanaume je atakapoachiwa mke (wa rafiki, ndugu au jirani) atamtongoza au la? Imeelezwa na baadhi ya watoataarifa wetu kwamba mke wa mtu ni rahisi kumhudumia kuliko mke wako. Hii ni kwa sababu mke huyo tayari ana mume wake ambaye ndiye mwenye jukumu la kumhudumia. Pia, inaelezwa katika msemo mwingine kwamba 'Mwanaume asiye na mchepuko ni sawa na taifa bila chama cha upinzani'. Mchepuko anaweza kuwa ni mpenzi wa nje ya ndoa wa kike au wa kiume, hata hivyo, msemo huu unamlenga hasa mwanaume. Kupitia msemo huu inaonekana kwamba wanaume ndio wanaopaswa kuwa na wapenzi wengi. Msemo huu hauoneshi kujali madhara ya mchepuko kama vile wanandoa kutengana, kuuana, ndoa kuvunjika, kuumizana na migogoro isiyoisha (Msongo, 2014). Msemo huu siyo tu unaonesha tabia ya wanaume kuwa na wapenzi wengi, bali unaonesha nafasi ya vyama vya upinzani kwa taifa. Umuhimu mmojawapo wa kuwa na vyama vya kisiasa vya upinzani ni kuleta demokrasia na kuchochea maendeleo ya nchi. Suala la mchepuko[7] ingawa linakemewa katika kampeni za kitaifa kwamba linachangia katika maambukizi ya UKIMWI (taz. Msongo, 2014), katika msemo huu linasisitizwa na kuonekana kuwa ni jambo la manufaa. Kwa mujibu wa watoataarifa wetu, mwanamke akiwa hana wake wenza anajisahau kutimiza wajibu wake wa masuala ya unyumba kwa mumewe. Jambo hili hata hivyo linahitaji utafiti zaidi.

Misemo mingine kuhusiana na tabia na wajihi ni 'Mwanaume haendi leba'[8]. Msemo huu unaonesha uhalisi wa kijinsi kibiolojia kwamba jukumu la kuzaa ni la mwanamke, si la mwanaume. Kuhusiana na wajihi kimavazi, inaelezwa kwamba 'Mwanaume ndevu' na 'Mwanaume suruali'[9]. Misemo hii inaonesha kwamba kuota ndevu na kuvaa suruali ni sifa ya mwanaume, si mwanamke. Suala la mwanaume pekee kuvaa suruali kwa sasa haliakisi ukweli wa maisha kwani hata mwanamke anavaaa pia. Hivyo, baadhi ya misemo hii inapaswa kutazamwa kwa jicho pevu zaidi lenye kuzingatia utamaduni wa dunia ya sasa wenye kuathiriana sana kutokana na kukua kwa utandawazi na kubadilika kwa mitazamo kuhusiana na mambo fulani.


### 3.1.1.4 Nafasi ya Wapenzi wengi

Misemo hii inaonesha kwamba jinsi zote mbili zinashiriki kuwa na wapenzi wengi, ingawa inatofautiana kimsisitizo. Misemo kama vile 'Kahaba hana mahaba', 'Wanakupenda sababu uko kwa mumeo ondoka uone' na 'Mkanye mkeo gari sio langu' inaonesha mwanamke ama wa ndani ya ndoa au la anavyoweza kuwa na wanaume wengi. Misemo hii miwili ya mwisho kimsingi inalenga kumuonya mwanamke kuachana na tabia hiyo. Mwanaume pia anasawiriwa kuwa ni laghai wa kimapenzi kwa kuwapenda wanawake walioko katika ndoa na pindi wakiachwa na waume wao naye huwakataa.

---

[7] Pia taz. tangazo Baki Njia Kuu, Mchepuko sio Dili. Epuka UKIMWI.
[8] Leba imetoholewa kutoka *labour ward* (wodi ya wazazi) hivyo hapa inamaanisha mwanaume haendi leba kuzaa kwani hilo ni jukumu la mwanamke.
[9] Maana nyingine ya msemo huu ni kwamba mwanaume ambaye hana kazi yoyote ya kumpa kipato bali anategemea uanaume wake tu.

Kwa upande wa wanaume, misemo kadhaa imedhihirika. Misemo hiyo ni 'Mwanaume asiye na mchepuko ni sawa na taifa bila chama cha upinzani', 'Mke mmoja hudumaza akili', 'Kitunze cha ndani hawara hana shukurani'[10] na 'Ogopa sana nyumba ndogo haili matembele.' Misemo miwili ya kwanza inahimiza mwanaume awe na mwanamke wa nje ya ndoa (mchepuko) au kuoa kabisa kwani mke mmoja atamfanya akili yake kudumaa. Suala la kuoa wake wengi linafanyika kidini, hususani ya Kiislamu na jadi, ingawa hapa msemo huu unaonesha kuwalenga wanaume wote bila ya kujali ni waumini wa dini gani. Msemo 'Mwanamke mmoja kudumaza akili ya mwanaume' haujathibitika kisayansi ila imeelezwa na baadhi ya watoataarifa kuwa mwanaume kuwa na wanawake wengi ni sifa na inaonesha urijali wake. Kwa kiasi fulani, msemo 'Mke mmoja hudumaza akili' unaonesha kwamba mwanamke hana mchango kiakili katika maamuzi mbalimbali katika ndoa au familia, na akiwa mmoja huweza hata kudumaza akili ya mume. Msisitizo wa wanaume kuwa na wanawake wengi wakati mwingine unaweza kuhamasisha kuenea kwa maradhi kama vile UKIMWI. Tafiti zinaonesha kuwa mojawapo ya mambo yanayoeneza UKIMWI ni kuwa na wapenzi wengi, kutotumia kondomu, kuchangia sindano na kadhalika (Mpondo, Gunda na Kilonzo, 2017). Misemo miwili ya mwisho inadokeza kuwa wanaume wana mahusiano na wapenzi wa nje ya ndoa. Hivyo, misemo hiyo inawaonya wanaume wasipende kuwa na vimada/nyumba ndogo kwani hata ukimfanyia mambo mazuri kiasi gani huwa hana shukurani na pia anapenda vitu vya gharama. Vielelezo vifuatavyo vinadhihirisha baadhi ya misemo hiyo.

|   |   |
|---|---|
| e. Mwanaume asiye na mchepuko ni sawa na taifa bila chama cha upinzani | f. Mke mmoja hudumaza akili |

***Kielelezo Na. 2: Msemo kwenye lori (e) na daladala (f)***

Kwa ujumla, misemo hii inahimiza mwanaume na mwanamke kutulia kwenye ndoa zao, mwanaume anahimizwa kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja, anaweza kuwa kimada au mke. Suala la usaliti na kukosa uaminifu katika mapenzi kwa jinsia zote mbili linajitokeza kwani, wote, mwanaume na mwanamke, wanaonekana kuwa na wapenzi wa nje ya ndoa zao.

[10] Ingawa hawara anaweza kuwa mwanamke au mwanaume, msemo huu unamlenga mwanaume kwani huchukuliwa kuwa ndiye hutunza/huhudumia mke na watoto.

### 3.1.1.5 Uwezo wa Kiuchumi na Umiliki Mali

Suala la umiliki mali pia limejitokeza katika misemo hii inayosawiri mapenzi na ndoa kwa jinsia zote mbili. Msemo mmojawpao ni 'Heri kukosea kujenga nyumba kuliko kukosea kuoa'. Msemo huu ingawa unasisitiza umuhimu wa kuoa unadokeza pia kwamba mwanaume ndiye hujenga na kumiliki nyumba. Mali nyingine inayomilikiwa na mwanaume kupitia misemo hii ni pesa na gari, mathalani, misemo mingine inasema 'Kama mapenzi ni pesa kaolewe na benki', 'Kuachwa na mwanamke anayependa hela ni sawa na kumaliza mkopo benki', 'Filisika ujue tabia ya mkeo', na 'Mkanye mkeo gari sio langu.' Misemo hii inaonesha si tu tabia ya mwanamke kupenda wanaume wenye mali kama vile pesa na gari na hata kumkataa mwanaume asiye na pesa, bali kwa upande mwingine inaonesha kuwa vitu hivyo humilikiwa na mwanaume. Mwanaume ndiye mmiliki wa mali na ndiye mwenye uwezo kiuchumi. Mwanamke anasawiriwa kuwa ni tegemezi anayeishi kwa kumtegemea mwanaume. Wakati mwingine, mke pia huonekana ni sehemu ya mali ya mume. Hili linadhihirika katika msemo 'Nikifa mke wangu asiolewe: usia uheshimiwe.' Katika ulimwengu wa leo unaotetea haki, mabadiliko na 'jinsia kama kipengele muhimu kwa maendeleo' (World Bank, 2012), mtazamo kwamba mwanamke ni tegemezi na ni mali ya mwanaume inabidi uachwe.

### 3.1.2 Mapenzi na Elimu kwa Mtoto wa Kike

Misemo kadhaa inazungumzia mapenzi na elimu/shule kwa mtoto wa kike pamoja na changamoto zake. Misemo hii inawalenga wanafunzi hususani wa kike na mingine inawalenga wanaume wanaopenda kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi hao na hata wazazi wa watoto hao. Misemo kadhaa inadhihirisha jambo hili, ikiwamo 'Kabadilishe uje'[11]. Msemo huu unamtaka mwanafunzi wa kike ambaye anatoka shuleni aende nyumbani akabadilishe sare za shule ili avae nguo za nyumbani na kisha aende kwa mwanaume husika ambaye anamtaka kimapenzi. Mwaka 2016, bunge la Tanzania lilipitisha marekebisho kwenye Sheria ya Elimu yaliyoeleza kwamba ikibainika kwamba mtu amempa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela[12]. Msemo huu unaonekana kusemwa na mwanaume mwenye tamaa ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi wa kike lakini wakati huohuo unaonesha woga alionao kwa kutembea na mwanafunzi huyo. Aidha, imebainika kuwa wanafunzi wa kike wanapenda kula chipsi. Msemo ambao unadhihirisha jambo hili ni 'Ukipenda chipsi usiogope mimba'[13]. Msemo huu unaonesha kwamba wanafunzi wa kike nchini hupata mimba wakiwa shuleni kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo umaskini (McCleary-Sills na wenzake, 2013) na kutaka zawadi kama vile pesa (Pincock, 2019) na chipsi.

---

[11] Katika gari ambalo limeandikwa msemo huu kuna pia picha ya mwanafunzi aliyevaa sare za shule.

[12] Asangama, Karume (2016) 'Sheria mpya nchini Tanzania, miaka 30 jela'. Katika https://www.rfi.fr/sw/eac/20160725-sheria-mpya-nchini-tanzania-miaka-30-jela

[13] Msemo mwingine unaofanana na huu ni 'Utamu wa chipsi mimba'.

Mimba za utotoni ni mojawapo ya sababu kubwa zinazofanya wasichana kuacha au kufukuzwa shule (Meena, 1996). Msemo ‘Ringa tena’[14] unamkebehi na kumcheka msichana aliyepata mimba (akiwa bado mwanafunzi). Msemo huu ni kama matokeo ya ‘Kabadilishe uje’ na ‘Ukipenda chipsi usiogope mimba’. Hata hivyo, badala ya msemo huu kumsikitikia binti huyo aliyejiingiza katika mahusiano ya kimapenzi akiwa bado mwanafunzi na hatimaye kupata mimba, msemo ‘Ringa tena’ unaonekana kumkebehi msichana huyu. Haijulikani anayesema hivi ndiye mwanaume aliyempa mimba msichana huyo au la. Kebehi hii labda inatokana na ukweli kwamba nchini Tanzania mwanafunzi wa kike wa shule ya msingi au sekondari akipata ujauzito hufukuzwa shule. Sheria hii imekuwapo tangu miaka ya 1960 (Pincock, 2019) na wadau wa elimu wamekuwa wakisisitiza ibadilishwe ili kutoa fursa kwa wasichana hao kuendelea kielimu. Hata hivyo, serikali mwaka 2021 ilitangaza kubadilisha sheria/sera hiyo na kuwaruhusu wanafunzi wa kike wa shule za msingi na sekondari wanaopata ujauzito kurudi shuleni chini ya mfumo rasmi wa elimu (Ng’ingo, 2021). Kwa ujumla, misemo hii inaonesha changamoto azipatazo mwanafunzi wa kike katika safari yake ya kielimu. Vielelezo vifuatavyo vinaonesha misemo hiyo.

<table>
<tr><td>
</td><td>
</td></tr>
<tr><td>g. Kabadilishe uje</td><td>h. Ringa tena</td></tr>
</table>

***Kielelezo Na. 3: Msemo kwenye bajaji (g) na bodaboda (h)***

Wanaume ambao wanapenda kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike pia wamezungumziwa katika misemo hii. Mathalani, kuna msemo ‘Kama sketi za wanafunzi zinakuchanganya kamshonee mkeo’. Tafiti kadhaa zimeonesha kuwa baadhi ya watu wazima wamekuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike wa

[14] Msemo huu umeambatana na picha inayoonesha msichana akiwa mjamzito.

shule za msingi na sekondari (Adolf, 2017). Msemo huu unalenga kumtetea mtoto wa kike na umetumika kama kejeli kwa wanaume hao kwamba kama kinachowavutia kwa wanafunzi wa kike ni sketi za shule wanazovaa, basi ni vema wakawashonee wake zao ili nao waonekane kama wanafunzi. Kimsingi, msemo huu unakemea tabia ya wanaume kutembea na wanafunzi wa kike kwani kunaweza kuwasababishia kupata mimba za utotoni, kuacha shule na kuwaharibia ndoto zao za maisha.

Msemo mwingine ni ule unaoona kwamba elimu kwa mtoto wa kike si muhimu kwani hatimaye ataishia kuolewa tu. Mtazamo huu ulitawala sana miaka ya nyuma na hata sasa katika baadhi ya maeneo na jamii nchini Tanzania kiasi hata cha baadhi ya wazazi kutotilia maanani elimu ya mtoto wa kike. Matokeo yake mtoto wa kiume ndiye hupata elimu ilhali mtoto wa kike anakuwa nyuma kielimu. Msemo 'Somesha aolewe' si tu unaonesha mtazamo hasi wa baadhi ya wanajamii kuhusu elimu kwa wasichana bali pia unakatisha tamaa wazazi au walezi ambao wanasomesha watoto wao wa kike. Aidha, mara kadhaa imekuwa ikiripotiwa watoto wa kike kuacha shule kwa sababu ya kupata mimba za utotoni, kuozeshwa, kufanya kazi ili kusaidia familia, umaskini na mazingira magumu ya shule (Lubasi, 2019). Vilevile, imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya wazazi kuwakatisha watoto wao wa kike masomo ili kuwaozesha kwa lengo la kupata mahari kama vile fedha na mifugo. Hata hivyo, wazazi wanaobainika huchukuliwa hatua na serikali ikiwamo kufungwa jela (Masasy, 2016; Mushi, 2020). Msemo huu unapingana na malengo ya nchi za SADC yanayosisitiza elimu kwa mwanamke na mtoto wa kike (SADC, 2016) na unapinga usawa wa kijinsia katika kufikia malengo ya milenia yanayoona kwamba mwanamke na msichana ni muhimu katika kuleta maendeleo. Aidha, msemo huu kwa mujibu wa Lazar (2007:144) unaonesha namna ambavyo 'ukosefu wa usawa wa kijinsia unavyodhihirika kupitia asasi mbalimbali' ndio maana 'UKTF unasisistiza haki ya jamii na mabadiliko katika masuala mbalimbali yahusuyo jinsia'.

### 3.2 Dhima ya Misemo hii kwa Jamii

Watoaji wengi wa misemo hii ni madereva na makondakta, wengi wao hawana muda wa kutosha kuandika matini kubwa zaidi kama vile vitabu. Hii ni kutokana na asili ya kazi yao, huanza kazi alfajiri sana na humaliza usiku. Hivyo misemo hii ni njia ya haraka ya kutoa na kufikisha ujumbe kwa walengwa wao na jamii kwa ujumla. Misemo iliyopo katika vyombo hivi vya usafiri inaibua fasihi tembezi (fasihi inayotembea) kando na ile ya vitabuni. Inaendeleza fasihi ya Kiswahili, kihadhira na kimbinu ya uwasilishaji, kwani jamii pana husoma au hulengwa na matini hizo. Kwa upande wa Afrika ya Mashariki, inaelezwa kwamba 'Misemo katika vyombo vya usafiri wa umma kama vile daladala, matatu, malori na bodaboda ni eneo muhimu la kutolea ujumbe. Ujumbe huo si tu unaburudisha, kuhabarisha na kuelimisha, bali pia una maana kijamii na kiutamaduni' (EAKC, 2019).

Misemo katika vyombo vya usafiri inaelimisha na kuasa jamii kuhusu masuala mbalimbali kama vile umakini katika kuchagua mwenzi wa kuoana naye na umuhimu wa ndoa katika jamii. Mathalani, jinsia zote mbili zinaaswa kutulia katika ndoa zake

('Wanakupenda kwa sababu uko kwa mumeo ondoka uone' na 'Kitunze cha ndani hawara hana shukurani'). Aidha, inawaasa wanafunzi wa kike kujiepusha na tamaa ambazo zinaweza kukatisha masomo yao kutokana na kupata mimba au kutozingatia masomo ('Ukipenda chipsi usiogope mimba'). Misemo hii pia inawaasa wanaume wanaopenda kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kwani wanaweza kuwakatisha wanafunzi ndoto zao za kimaisha na kusababisha kuongezeka kwa mimba za utotoni ('Kama sketi za wanafunzi zinakuchanganya kamshonee mkeo') na wao kuishia jela. Vilevile, wasichana na wanawake wanaaswa kuacha kutoa mimba kwani 'Kutoa mimba haikufanyi kuwa msichana bali utabaki kuwa mama wa marehemu'. Suala la utoaji mimba katika jamii yetu si tu ni kinyume na katiba ya nchi bali pia linakiuka maadili ya kidini na kiutamaduni wa Kiafrika ambao unasisitiza uzazi kwa ustawi wa jamii.

Misemo hii pia inawasilisha mitazamo ya baadhi ya wanaume kuhusu mambo kadhaa katika jamii. Mtazamo hurejelea namna matini inavyowasilisha imani za kiitikadi kupitia kwa mhusika au mwandishi wa kazi husika (Wamitila, 2008). Mathalani, katika misemo hii, mambo hayo ni pamoja na aina ya wanawake wa kuoa, kuna wanaume wengine wanaona mwanamke wa kuoa awe mweupe, mzuri wa sura au mwenye tabia nzuri. Misemo mingine inaona ni muhimu wanaume kuwa na wapenzi/wake wengi. Mathalani, inaaminika kupitia misemo hiyo kwamba mke mmoja hudumaza akili na mwanaume hupaswa kuwa na mchepuko (mwanamke wa nje ya ndoa). Aidha, inaoneshwa kwamba mmiliki wa mali ni mwanaume na mtoto wa kike hapaswi kupata elimu kwani uga wake ni ndoa. Mtazamo unaojitokeza katika misemo hii ni kwamba kwa mwanaume ni sifa kuwa na wapenzi wengi na pia ndiye anayepaswa kupata elimu rasmi. Siku hizi wapo pia makondakta wa kike, hata hivyo, idadi ndogo ya wanawake katika vyombo vya usafiri vya umma (kama vile madereva, makondakta na waandishi wa misemo hiyo) inaweza kuchangia kuwapo kwa misemo mingi inayoandikwa humo kuwakilisha mtazamo na raghba za wanaume. Kama Case (1992) asemavyo kwamba 'misemo na stika za kwenye bampa za magari inawapa watu fursa ya kutoa mitazamo yao, kuonesha utambulisho wao, raghba zao na thamani ya vitu mbalimbali'.

Pia misemo hii inasawiri na kuwasilisha utamaduni wa jamii. 'Utamaduni ni jinsi watu wanavyoishi, imani zao, maadili, itikadi, dini na desturi zao za jamii' (Meena, 1996:46). Mojawapo ya asasi ya utamaduni iliyoongelewa kwa kina na misemo hii ni ndoa. Mambo yaliyoongelewa ni umuhimu wa kuteua kwa umakini mwenzi wa kuoa/kuolewa naye, wanaume kuwa na wake wengi na thamani ya mwanamke mweupe au mwenye tabia nzuri. Mathalani, kwa mujibu wa watoataarifa wetu imebainika kwamba baadhi ya jamii nchini hutoza mahari kubwa kama binti anayeolewa ni mweupe. Aidha, misemo hii inaendeleza kwa kiasi kikubwa imani kwamba mwanamke bado ni kiumbe tegemezi kiuchumi na mwanaume ndiye mmiliki mali. Jambo hili si sahihi sana kwani kwa sasa wanawake wengi wanashiriki katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo na kujikwamua kiuchumi na hata kuwapita baadhi

ya wanaume. Misemo hii inaendeleza 'itikadi tawala ya kiume inayotumia utamaduni kuhalalisha mahusiano kandamizi ya kijinsia' (Meena, 1996:46). Akizungumzia matini za teksi nchini Afrika Kusini, Rassmann (2004) naye anaeleza kuwa teksi ni sehemu ya sanaajadiya *(folklore)* za mjini na ni uga wa kutolea maoni na kuakisi maisha na utamaduni wa jamii husika.

Kadhalika, misemo hii inaendeleza usaguzi wa kijinsia *(gender stereotypes)* katika jamii. Usaguzi wa kijinsia ni mawazo mgando kuhusiana na nafasi, utambulisho, majukumu na sifa ambazo mtu wa jinsi ya kike na ya kiume hupewa na jamii na hatimaye kuchukuliwa kwamba, ndivyo zilivyokuwa, ndivyo zilivyo na zinatakiwa ziwe au zibaki hivyo bila kubadilika kizazi baada ya kizazi (Lyimo, 2014). Misemo hii inamsawiri mwanamke kwamba ndiye mwenye tabia mbaya, mpenda ngono na ni tegemezi kiuchumi. Mwanaume anasawiriwa kuwa ana tabia nzuri (ndiye anayepaswa kurekebisha tabia mbaya ya mwanamke), mwenye fahari ya kuwa na wapenzi/wake wengi na anajiweza kiuchumi na kimaendeleo (ana nyumba, gari, pesa na mkopo wa benki). Usawiri huu katika kazi za fasihi, kama inavyoelezwa na Lazar (2005) na Shehzad (2013) unaendeleza usaguzi na upendeleo wa kijinsia na unaakisi mfumodume kwa kuendeleza utawala wa kiume. Hali hii huweza kutokana na kwamba watendaji wengi katika vyombo vya usafiri (yaani madereva, makondakta na waandishi wa misemo hiyo) ni wanaume (taz. pia Wa-Mungai, 2003; Joshua, 2013).

Kadhalika, misemo ya kwenye vyombo vya usafiri inaendeleza usawiri uliozoeleka wa mwanamke na mwanaume katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Usawiri uliozoeleka katika kazi za fasihi unamsawiri mwanamke kwa upande hasi kuliko chanya na kumsawiri mwanaume kwa upande chanya kuliko hasi (taz. pia Mbughuni, 1982; Ngongolo, 2015). Mathalani, katika misemo hii mwanamke anasawiriwa kuwa ni mpenda ngono, tegemezi, mchuna pesa za wanaume, hana uwezo kiakili wa kuleta maendeleo (akiwa mmoja hudumaza akili ya mume) na ana tabia mbaya. Mwanaume anasawiriwa kuwa ni mwenye mamlaka, mmiliki mali, na ana pesa. Udunishaji wa mwanamke na ukwezaji wa mwanaume katika matini hizi ungeweza kubadilika kwani jinsia hujengwa kijamii, 'hautokani na tofauti ya kibailojia na wala haupaswi kudumu milele' (UNESCO, 2003:1).

Misemo hii pia inaonesha ukweli fulani wa maisha katika jamii. Mambo mengi yaliyozungumziwa katika misemo hii si mapya. Mathalani, tamaa na ulaghai wa mapenzi kwa wanawake na wanaume.

## 4.0 Hitimisho

Makala imebaini kwamba baadhi ya misemo ya kwenye vyombo vya usafiri inawasilisha dhamira mbalimbali kwa mrengo wa kijinsia. Dhamira hizo ni pamoja na mapenzi na ndoa, elimu, na kadhalika. Suala la mapenzi na ndoa limejitokeza sana kwani watendaji wengi wa uwanja huu hasa madereva na makondakta ni vijana. Hivyo, misemo inawasilisha mawazo yao yenye kusawiri maisha, matamanio, raghba na utamaduni wa jamii. Kwa ujumla, misemo hiyo inalenga kusawiri jinsia zote mbili ingawa kwa msisitizo tofauti. Tofauti na mwanaume, mwanamke hakusawiriwa kama

ni kiumbe mwenye kupiga hatua kimaendeleo, jambo ambalo halina ukweli sana na hivyo linapaswa kubadilishwa. Aidha, misemo hiyo ina dhima muhimu kiutamaduni kwani inasawiri mambo ambayo yamo katika jamii, mila na desturi za jamii. Misemo hii inaelimisha, inakosoa, inaasa, inashauri na inaelekeza baadhi ya mambo katika jamii na kusawiri ukweli fulani wa maisha.

## Marejeleo


Ackermann, D. (1991). *Being Women Being Human, Women Hold up Half the Sky: Women in the Church in South Africa*. Pietermaritzburg: Cluster Publications.

Adolf, G. (2017). "Mwalimu Ampa Mimba Mwanafunzi wake", *Nipashe* la tarehe 21 Julai.

Case, C.E. (1992). "Bumper Stickers and Car Signs Ideology and Identity". *Journal of Popular Culture*, 26 (3): 179-190.

Erlurk, Y. (2004). "Reconsidering the Role of Men in Gender Agenda Setting: Conceptual and Policy Issues". *Feminist Review*, 78: 3-12.

East African Kiswahili Commission (EAKC). 2019. *Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC*. Zanzibar: East African Kiswahili Commission.

Howard, J.E. and Rackin, P. (2002). *Engendering a Nation: A Feminist Account of Shakespeare's English Histories*. London: Taylor and Francis.

Joshua, G. (2013). "Heroes of the Road: Race, Gender and the Politics of Mobility in Twentieth Century Tanzania." *Africa: Journal of the International African Institute*, 83(3):403-425.

Kabaka, D. (n.d). 'Msichana wa Elimu,' Nairobi: Daudi Kabaka Beats katika https://www.youtube.com/watch?v=2Sp8OUX4pMQ imesomwa tarehe 25/12/2020.

Kaijage, S. (2016). "Misemo na Maneno mbalimbali Yaliyoandikwa katika Magari, Bajaji na Pikipiki." katika http://stanleykaijage.blogspot.com/2016/03/misemo-na-maneno-mbalimbali.html. Makala imesomwa tarehe 1/1/2021.

Katambi, A. (2021). Matumizi ya Lugha Yanavyosawiri Mfumodume katika Nyimbo za Taarab za Wasanii wa Kike Nchini Tanzania. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Lawuyi, O.B. (1997). "The World of the Yoruba Taxi Driver: An Interpretive Approach to Vehicle Slogans". In K. Barber (Ed.) *Readings in African Popular Culture*. London: James Currey. pp. 1-13.

Lazar, M.M. (ed.). (2005). *Feminist Critical Discourse Analysis: Gender, Power and Ideology in Discourse*. London: Palgrave.

______(2007). "Feminist Critical Discourse Analysis: Articulating a Feminist Discourse Praxis". *Critical Discourse Studies*, 4(2):141:164.

Ligaga, D. (2020). *Women, Visibility and Morality in Kenyan Popular Media*. Grahamstown: NISC (Pty) Ltd.

Lubasi, S. (2019). "Sababu za Wasichana Kuacha Shule Zabainishwa," *HabariLeo* la 15/03/2019, https://habarileo.co.tz/habari/2019-03-155c8b42dc898cd.aspx. Imesomwa tarehe 28/12/2020.

Lyimo, E.B. (2014). Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau Nchini Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mahenge, E. (2009). "Uchambuzi wa Fani na Maudhui katika Semi Zilizopo kwenye Tiketi za Daladala: Mifano kutoka kwenye Daladala za Dar es Salaam". *Kioo cha Lugha*, 7:51-67.

Malima, C.C. (2018). Kuchunguza Matumizi ya Misimu ya Wanavyuo Inavyotumika katika Mitandao ya Kijamii Mjini Morogoro. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Masasy, K. (2016). "Mwanafunzi Aliyeolewa kwa Nguvu Arudishwa kwao," *HabariLeo* tarehe 4/2/2016. https://www.habarileo.co.tz/habari/mwanafunzi-aliyeolewa-kwa-nguvu-arudishwa-kwao.aspx. Imesomwa tarehe 28/12/2020.

Mbilinyi, M. (2000). "Gender Issues in Higher Education and their Implications for Gender Mainstreaming and Strategic Planning." University of Dar es Salaam: Gender Dimensions Programme Committee.

Mbiti, J.S. (1995). *African Religion and Philosophy*. London: Heinemann.

Mbughuni, P. (1982). "The Image of Women in Kiswahili Prose Fiction." *Kiswahili*, 49(1):15-24.

McCleary-Sills J, Douglas Z, Rwehumbiza A, Hamisi A, and Mabala R. (2013). "Gendered Norms, Sexual Exploitation and Adolescent Pregnancy in Rural Tanzania". *Reproductive Health Matters*, 21(41): 97-105.

Meena, R. (1996). "Situational Analysis of Education of Girls/Women in Tanzania." *UTAFITI*, 3(2):39-90.

Mosha, E.S. (2013). Discourse Analysis of Gender - Based Violence in Contemporary Kiswahili Fiction: A Case Study of Selected Novel of the Past Three Decades (1975 - 2004) and Young Tanzanians' Interpretation. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Waikato, New Zeland (Haijachapishwa).

Mosha, D.F. (2019). Ulinganishi wa Majukumu ya Wahusika Kijinsia katika Nyimbo za Watoto na Uhalisia wake katika Malezi ya Watoto Nchini Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mpondo, B.C.T, Gunda, D.W, and Kilonzo, S.B. (2017). HIV Epidemic in Tanzania: The Possible Role of the Key Populations." *Hindawi: AIDS Research and Treatment*, 1-8.

Msongo, B. (2014). ''Michepuko' Inavyozivurga Ndoa', katika *HabariLeo* 12/04/2014. https://habarileo.co.tz/habari/michepuko-inavyozivuruga-ndoa.aspx. Imesomwa tar. 20.8. 2019.

Mturo, N.G. (2011). Dhima ya Semi Zilizoandikwa kwenye Daladala: Uchambuzi wa Vipengele vya Lugha na Dhamira. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mushi, J. (2020). "Baba Aliyetaka Kuozesha Mwanafunzi wa Miaka 12 Atiwa Mbaroni Arusha", Mtanzania Digital, tarehe 15/06/2020.

Ng'ingo, E. (2021). 'Waipongeza Serikali Kuruhusu Wanafunzi Wanaopata Ujauzito' katika https://habarileo.co.tz/habari/2021-11-2661a074dd29dc2.aspx. Imesomwa tarehe 16/12/2021.

Ngongolo, M.J. (2015). Usawiri wa Mwanamke katika Hadithi za Magazeti ya Udaku. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Omari, S. (2011). Poetics of *Daladala*: The Case of HIV/AIDS Dialogue in *Daladala* Ticket Slogans. *Kiswahili*, 74:78-94.

Pincock, K. (2019). 'Tanzanian Girls Need Support, not Threats, to avoid Pregnancy' katika https://theconversation.com/tanzanian-girls-need-support-not-threats-to-avoid-pregnancy-126540. Imesomwa tarehe 3/6/2020.

Rassmann, E. (2004). "Taxi Texts as Reading Material and a Source of Cultural Schemata for L2 Zulu". *Southern African Linguistics and Applied Language Studies*, 22(3-4):143-157.

SADC. (2016). *SADC Gender and Development Monitor. Gaborone: SADC, SARDC.*

Schiffrin, D. (2006). "Discourse" in Fasold, Ralph, W & Jeff Connor-Linton (eds) *An Introduction to Language and Lingusitics*. Cambridge: Cumbridge University Press. pp. 169-203.

Sen, G., George, A., and Piroska őstlin. (2002). *Engendering International Health: The Challenge of Equity*. Massachusetts: Massachusetts Institute of Technology.

Shehzad, A. (2013). "Understanding Gender Politics in Literature: A Study of the Tenant of Wildfell Hall by Anne Bronte". *Mediterannean Journal of Social Sciences*, 4(11):734-737.

TLS. (2015). *Ijue Sheria ya Urithi, Mirathi na Wosia*. Dar es Salaam: Chama cha Wanasheria Tanzania Bara.

UNESCO (2003). "Gender Mainstreaming Implementation Framework". https://unesdoc.unesco.org . Imesomwa tarehe 20/7/2019.

Wamitila, K.W. (2003*). Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

______(2008*). Kanzi ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide ~ Muwa Publishers Limited.

Wa-Mungai, M. (2003). Identity Politics in Nairobi Matatu Folklore. PhD Thesis. The Hebrew University of Jerusalem.

Waylen, G. (2007). *Engendering Transitions: Women's Mobilization, Institutions, and Gender Outcomes*. New York: Oxford University Press Inc.

World Bank (2012). World Development Report 2012: Gender Equality and Development.

World Bank. https://openknowledge.worldbank.org/handle/10986/4391. Ripoti

Imesomwa tarehe 9/7/2020.

**Kiambatisho: Misemo husika**

1. Mapenzi bila uongo humpati mtu.
2. Ajali si kugongwa na gari tu hata ukikosea kuoa/kuolewa, nayo ni ajali.
3. Heri kukosea kujenga nyumba kuliko kukosea kuoa.
4. Usichague mke kwenye sherehe.
5. Mtalaka wa huku ndo mke mpya wa kule.
6. Kuachwa na mwanamke anayependa hela ni sawa na kumaliza mkopo benki.
7. Nikifa mke wangu asiolewe: usia uheshimiwe.
8. Kuoa mke mweupe ni kama kupanda miwa eneo la shule.
9. Kuoa mke mzuri ni sawa na kulima miwa eneo la shule.
10. Kuoa mke mzuri ni sawa na kulima shamba la miwa karibu na shule.
11. Uzuri wa mwanamke tabia, sura hata mbuzi anayo.
12. Mwanamke sura tabia nitamnyoosha.
13. Filisika ujue tabia ya mkeo.
14. Kahaba hana mahaba.
15. Ukitaka kumjua mume mwenzio, muachie mkeo.
16. Kama mapenzi ni pesa kaolewe na benki.
17. Usinichune sana nina watoto.
18. Kama mzuri olewa.
19. Wanakupenda kwa sababu uko kwa mumeo ondoka uone.
20. Kitunze cha ndani hawara hana shukurani/Tunza wa ndani hawara hana shukrani.
21. Kutoa mimba haikufanyi kuwa msichana bali utabaki kuwa mama wa marehemu.
22. Mkanye mkeo gari sio langu.
23. Mke mmoja hudumaza akili.
24. Mke si ndugu.
25. Mwanaume asiye na mchepuko ni sawa na taifa bila chama cha upinzani.
26. Mwanaume haendi leba.
27. Mwanaume ndevu.
28. Mwanaume suruali.
29. Nyumba ndogo haili matembele.
30. Ogopa sana nyumba ndogo haili matembele.
31. Kabadilishe uje.
32. Ukipenda chipsi usiogope mimba.
33. Utamu wa chipsi mimba.
34. Ringa tena.
35. Somesha aolewe.
36. Kama sketi za wanafunzi zinakuchanganya kamshonee mkeo.